



HALMASHAURI YA JIJI ARUSHA



Barua zote zitumwe kwa:
Simu: +255 27 2548072/2503494
(Director) +255 27 2544330 (General)
Nukushi: +255 27 2545768
Unapojibu tafadhali taja:

Mkurugenzi wa Jiji
S. L. P. 3013,
20 Barabara ya Boma,
23101 ARUSHA,
BaruaPepe:
cjj@arushacc.go.tz
Tovuti: www.arushacc.go.tz
Tarehe: 13 Februari, 2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha anawatangazia nafasi za ajira ya muda kwa ajili ya kazi ya kukusanya taarifa na kutekeleza zoezi la uwekaji wa anwani za makazi katika kata ya

1. SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 – 35
- Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- Awe anamiliki simu janja yenye Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa muda mrefu
- Awe na barua pepe inayotumika
- Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa
- Awe ni mkazi wa kata husika
- Awe mwaminifu na mwadilifu anayeweza kufanya kazi kwa kujituma na kuzingatia muda uliowekwa

2. KAZI NA MAJUKUMU

- Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kutumia anwani za makazi
- Kuandika namba za anwani kwenye nyumba/majengo


d) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wa kazi

3. MAELEKEZO YA JUMLA

- a) Malipo kwa mwezi itakuwa ni Tshs. 300,000/=
- b) Maombi yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma pamoja na nakala 2 za picha (Passport size)
- c) Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni 19.02.2022 saa 4:00 asubuhi

4. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa usahihi zikionesha anuani kamili ya muombaji, namba za simu pamoja na barua pepe na ziwasilishwe ofisini kwa Mtendaji wa Kata husika ikiwa katika bahasha iliyofungwa.


John M. Pima (Ph.D)

MKURUGENZI WA JIJI